Nuru ya Kiswahili, Juzuu 3(1), Juni 2024: 27-42
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru31.2742

# Mbinu za Kukabiliana na Utamaushi katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganisho wa Wimbo Teule wa Jux na Diamond Platnumz na Kazi Teule za Kezilahabi

**Alfred Malugu**
**Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Rongo**
alfredmalugu@yahoo.com

**na**

**Caesar Jjingo**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Makerere**
caessarial@gmail.com

**Ikisiri**
Makala hii inakusudia kuonesha namna utamaushi unavyojitokeza katika wimbo wa "Enjoy" na kazi teule za Kezilahabi. Kutokana na maisha kuonekana kama kitu cha kukatisha tamaa (kutamausha) kwa kadri yalivyogubikwa na madhila mbalimbali, wimbo wa "Enjoy" unaonesha kuwa suluhisho ni kuamua "ku-*enjoy*" (kuyafurahia tu) kwa kadri mtu anavyoweza baada ya kupata nafasi ya kufanya hivyo. Hii ni tofauti na ilivyo katika kazi zingine za kidhanaishi, hususani kazi za Kezilahabi, ambazo zinaonesha kuwa suluhisho ni kujiua. Nadharia ya Udhanaishi iliongoza katika uchambuzi wa matini teule. Mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumika katika kupata data zilizofanikisha makala hii. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini. Matokeo ya utafiti uliozaa makala hii yanaonesha kuwa maisha ayaishiyo mwanadamu ni mafupi, mwanadamu anao uhuru wake binafsi, kuna kukata tamaa kunakosababishwa na masuala ya mapenzi, dunia ni uwanja wa fujo—kila mtu amekuja kufanya fujo zake na mwisho atajiondokea, na, mwisho, masuala ya mahusiano ya kimapenzi ni huzuni tupu. Makala inahitimisha kwa kutoa mapendekezo kuwa

suluhu ya kukata tamaa maishani siyo kujiua bali kuyafurahia maisha kwa kadri mtu awezavyo kwani kujiua hakutatui tatizo husika bali huweza kusababisha tatizo ama matatizo mengine. Aidha, iwapo mwanadamu ataamua kufanya fujo zake, ni vema afanye fujo za amani zisizowaathiri wengine. Uhuru binafsi uzingatie mipaka, kwani kila kitu kinapopitiliza huweza kuwa na madhara.

**Dhana za Msingi:** utamaushi, udhanaishi, Bongo fleva

## Utangulizi

Maana na thamani ya maisha ni miongoni mwa maudhui yanayowasilishwa na kazi mbalimbali za fasihi. Makala hii inajadili suala la udhanaishi kama linavyodhihirika katika wimbo wa "Enjoy" na kazi za mwandishi Euphrase Kezilahabi. Kidashari (2014) anaeleza kuwa udhanaishi ni mtazamo wa kifalsafa unaomfanya mwanadamu achambue maana, kiini, na thamani ya maisha. Udhanaishi hujaribu kuhoji maswali kama vile: Binadamu ni nani? Maisha ni nini? Na, nini maana ya kifo? Katika kuishi kwake, binadamu hukutana na mambo mengi yanayofurahisha, kuhuzunisha, na hata kukatisha tamaa. Hali ya ukataji tamaa ndiyo inayonasibishwa na dhana ya utamaushi.

Wasanii mbalimbali—wa fasihi simulizi na fasihi andishi—husawiri kwa namna tofauti masuala yanayomzonga binadamu katika kuishi kwake. Pamoja na kujadili suala moja la kuishi kwa mwanadamu, wasanii hao hutofautiana katika kuyafasiri maisha, hatimaye, hutofautiana pia katika kutoa suluhisho la matatizo yanayomzonga mwanadamu katika maisha yake. Makala hii inajadili tofauti hizo kwa kuangazia namna wasanii Jux na Diamond Platnumz, kupitia wimbo wa "Enjoy", wanavyoyafasiri maisha na suluhisho lao kuhusu mazonge yanayotokana na maisha, huku fikra hizo zikilinganishwa na za Euphrase Kezilahabi kupitia kazi zake mbalimbali.

"*Enjoy*" ni neno la lugha ya Kiingereza ambalo, kwa lugha ya Kiswahili, linaweza kutafsiriwa kama "furahia." TUKI (2010) inafafanua neno furahia kuwa ni kujawa furaha, na neno "furaha" kama ukunjufu wa moyo, uchangamfu, ufurufu, bashasha, ucheshi au hali ya kuridhika ama hali ya kustarehe. Ni kutokana na neno hili "*enjoy*", ambapo mwanamuziki wa muziki wa kizazi kipya anayejulikana kwa jina la Juma Mussa na la kisanii kama Jux alipomshirikisha msanii mwingine kutoka katika kundi la Wasafi Classic Baby (WCB) ajulikanaye kwa jina la Nasib Abdul na la kisanii kama Diamond Platinumz kuimba wimbo huu. Hawa ni wasanii wa muziki wa kizazi kipya ujulikanao kama Bongo fleva.

Bongo fleva hujumuisha aina mbalimbali za nyimbo ambazo hupatikana Tanzania kama vile *Hip hop*, *Rap*, *RnB*, *taarabu*, *charanga*, *rhumba*, *raga*, *ngoma asili* na *zuku* (Omari, 2009; Mahenge, 2010 na Samwel, 2012). Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa nyimbo za Bongo fleva ni maarufu na zinakubalika katika jamii (Omari, 2009; Kadallah, 2010 na Samwel, 2012). Kukubalika kwa nyimbo hizi kunatokana na maudhui yanayowasilishwa na namna ya uimbaji wake. Kama sehemu ya utanzu wa ushairi simulizi, wimbo huu nao haujaepuka dhima za kifasihi, zikiwamo kuelimisha na kuburudisha.

Zipo tafiti mbalimbali ambazo zimekwishakufanywa kuhusiana na nyimbo za Bongo fleva. Tafiti hizi zimezitazama nyimbo za Bongo fleva kuwa ni sawa na fasihi pendwa ambayo kwa miaka ya hivi karibuni imeweza kuzikonga nyoyo za wengi wanaozifuatilia. Miongoni mwa wataalamu walioshughulikia na kuthibitisha kuwa Bongo fleva ni miongoni mwa tanzu pendwa kwa sasa ni Omari (2009). Mtaalamu huyu alishughulikia mambo yaliyochochea nyimbo za *Hip Hop* ya Kiswahili kuwa miongoni mwa fasihi

pendwa kama ilivyo kwa tanzu nyingine, hususani riwaya na tamthiliya. Utafiti wa Omari (keshatajwa) ulibaini kuwa kupendwa kwa nyimbo za *Hip Hop* ambazo ni miongoni mwa nyimbo za Bongo fleva kunasababishwa na mitindo na matumizi ya lugha pamoja na vipengele vingine vya kifani na kimaudhui. Aidha, kwa muda mrefu, nyimbo hizi zimekuwa zikitoa elimu kwa jamii. Miongoni mwa wataalamu wanaothibitisha nafasi maridhawa ya nyimbo za Bongo fleva ni Lupokela na Msuya (2010). Kwa pamoja, wanadai kuwa Bongo fleva ina jukumu la kutoa maadili na malezi katika nyanja za ndoa, elimu, siasa, lugha na UKIMWI.

Kwa upande wake, Euphrase Kezilahabi, ana mtazamo mwingine kuhusu maisha na masuluhisho ya matatizo yanayohusiana nayo. Wamitila (1998) anabainisha kuwa Kezilahabi anayaona maisha kama dubwana lisilo na maana, na kwamba, mwanadamu amekuja duniani kuteseka. Anaongeza kuwa wahusika wa kazi nyingi za Kezilahabi wamesawiriwa wakiwa wamechanganyikiwa au kukata tamaa kutokana na mazonge mbalimbali ya maisha. Hii ndiyo sababu inayofanya wahusika hao, hasa wakuu, waishie kwa vifo—tena vya kujinyonga.

Katika makala hii, mtazamo huu wa Euphrase Kezilahabi kuhusu maisha na namna ya kuyakabili umejadiliwa kiulinganishi na ule unaosawiriwa na Jux na Diamond Platinumz. Lengo la mjadala huu ni kuonesha mikinzano ya kimtazamo kuhusu dhana ya udhanaishi katika maisha na kupendekeza mtazamo unaofaa kufuatwa.

**Nadharia ya Utafiti**

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Udhanaishi. Hii ni nadharia iliyoshika kasi sana katika mataifa ya Kimagharibi wakati wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Katika kipindi hiki, maisha yalionekana kutokuwa na

maana, hasa kwa ajili ya ugumu wake na kuvunjika kwa maadili ya kijamii. Matumaini ya watu wengi yalipotea hata ikafikia watu wengine, kutokana na madhila waliyokuwa wanapitia, kupoteza matumaini maishani na wengine kufikia hatua ya kudai kwamba Mungu amekufa kwa sababu, kama angalikuwa hai, asingeruhusu kuteseka kama walivyokuwa wakiteseka. Wadhanaishi humchukulia binadamu kama chanzo cha ulimwengu. Hivyo, asingekuwapo hata ulimwengu nao usingekuwapo (Sakkos, 2008). Maudhui yanayowashughulisha wadhanaishi ni kama vile kifo, uhuru wa mtu binafsi, wajibu wa binadamu duniani, ubinafsi, kukata tamaa, na udhaifu wa kibinadamu.

Kulingana na Njogu & Chimerah (1999), kitovu cha mtazamo au falsafa hii kimekitwa katika maswali kuwa: Maisha ni nini? Yana maana gani kwa binadamu? Ni kwa njia gani mwanadamu anaweza kuyaboresha maisha yake yaliyojaa dhiki, mashaka na huzuni? Kuna haja gani ya kujisumbua na maisha iwapo hatima yake ni kifo? Msingi wa nadharia hii unafungamanishwa na mwanafalsafa Soren Kierkegaard (1813 - 1855). Katika kazi zake mbalimbali kama vile *Fear and Trembling* (1844), *The Concept of Anxiety* (1844) na *Sickness unto Death* (1049) aliuliza maswali kama vile: Maisha ya binadamu yana maana gani? Na je, kuna lengo gani katika maisha ya binadamu? Kwa mujibu wa mwanafalsafa huyu, inakuwa vigumu kuyakinisha kuwako au kutokuwako kwa Mungu kwa kuwa maarifa aliyo nayo binadamu yana kikomo. Nadharia ya Udhanaishi inaongozwa na mihimili minane ifuatayo:

(a) Maisha ni kifo cha polepole: kifo huanza mwanadamu anapozaliwa (mwanadamu huanza kufa pale tu anapozaliwa).

(b) Suala la kuwako au kutokuwako kwa Mungu: katika mhimili huu, kuna mjadala unaohoji ikiwa Mungu yupo au hayupo, na kama yupo

mbona watu wanapata shida na hawana msaada, au Mungu yupo kwa ajili ya nani.

(c) Dhana ya uhuru binafsi: Je, uhuru wa mtu binafsi upo au haupo? Kwa maana nyingine: je, ni kweli mwanadamu anao uhuru au uhuru wake unadhibitiwa?

(d) Maisha hayana maana: mwanadamu amekuja duniani kupata taabu na mateso; hivyo, dunia haina maana wala huruma kwake.

(e) Kukata tamaa: katika kazi za kidhanaishi, wahusika wanaishia kukata tamaa baada ya kukumbwa na changamoto mbalimbali za maisha.

(f) Dunia ni uwanja wa fujo: kila mtu amekuja duniani kufanya fujo zake na, baadaye, atajiondokea na kuwapa nafasi wengine nao waje wafanye fujo zao.

(g) Suluhisho la maisha yaliyokosa maana ni kifo. Wahusika wa kidhanaishi wanaishia kujiua kutokana na kukata tamaa ya maisha.

(h) Ndoa ni huzuni tupu: kukiwa na chembechembe za furaha basi ni kidogo sana.

Makala yetu imetumia mihimili mitano tu kati ya minane tuliyoiorodhesha katika kuchambulia na kuwasilishia data. Mihimili iliyotumika ni mhimili (a), (c), (d), (f) na (h). Mhimili (a) umetumika kudhihirisha namna maisha yanavyochukuliwa kuwa mafupi. Mhimili (c) umetumika kuonesha suala la uhuru wa mtu binafsi kuwa lipo ama halipo. Mhimili (d) umetumika kuonesha suluhu ya maisha yanayokatisha tamaa. Mhimili (f) unaonesha namna dhana ya fujo inavyojidhihirisha katika wimbo husika. Na mhimili (h) unaonesha namna ndoa na mahusiano ya kimapenzi yanavyosababisha huzuni na kukatisha tamaa.

**Methodolojia**

Data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini. Matini zilizotumika ni wimbo wa "*Enjoy*" wa Jux na Diamond Platinumz ukilinganishwa na kazi za Euphrase Kezilahabi ambazo ni *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), *Karibu Ndani* (1988), na *Dhifa* (2008). Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa maudhui. Ulinganisho ulilenga kudhihirisha namna udhanaishi unavyojitokeza na kufasiriwa kwa namna tofauti katika katika kazi hizo.

**Matokeo ya Utafiti**

Kulingana na utafiti wetu, tulibaini matukio na maelezo mbalimbali ndani ya wimbo yanayodhihirisha kuwapo kwa udhanaishi. Matukio haya, baada ya kubainishwa, yalishadidiwa na mihimili ya kidhanaishi na mawazo ya wataalamu mbalimbali wanaofungamanishwa na mwelekeo huu.

Kwanza kabisa, Jux na Diamond Platinumz wanaona kuwa namna ya kukabiliana na maisha mafupi ni bora "*kuenjoy*". Tukiwanukuu katika wimbo husika, wanasema:

> Bora ni *enjoy*,
> **Maisha mafupi ni *simple***
> Ya nini niteseke roho?
> Jiunge nami upoze koo (Kiitikio)

Mstari wa pili katika kiitikio unaeleza kuwa maisha ni mafupi. Kwa kuwa maisha yenyewe ni mafupi, haina haja ya kuteseka roho; badala yake, ni '*kuenjoy*' (kuyafurahia). Kuyafurahia maisha kunakosisitizwa na wasanii hawa ni kwa kunywa vinywaji (kupoza koo), hususani vyenye vilevi. Wimbo huu unaeleza namna dunia ilivyo na mambo mengi. Wingi huu wa mambo ndiyo chanzo cha kusababisha *stress* (kukosa utulivu wa akili).

Misukosuko ya mapenzi ni mojawapo ya mambo yanayoonekana kuchochea hali hii ya kukosekana kwa utulivu wa akili. Waimbaji wa wimbo huu wanaonesha kuwa, licha ya kuwapo kwa mambo mengi duniani, maisha ayaishiyo mwanadamu ni mafupi. Kwa kuwa maisha yenyewe ni mafupi, waimbaji hawa hawaoni ni kwa nini mwanadamu aitese roho yake. Wanaona kwamba, kama inawezekana, basi ipo haja ya kuyafurahia maisha (kupoza koo). Kwa muktadha wa video ya wimbo huu, suala la "kupoza koo" linahitaji mtu awe na uchumi wa kuruhusu kufanya hivyo. Suala hili linaweza kuwa changamoto ikiwa vipato vya watu wanaosisitiziwa "*kuenjoy*" ni vya "akina baba kabwela" ama "wenye kipato cha mkia wa mbuzi".

Mawazo haya ya Jux na Diamond Platnumz yanafungamana na mhimili wa udhanaishi unaoyatazama maisha kama kifo cha polepole ambacho huanza tu mwanadamu anapozaliwa (mwanadamu huanza kufa pale tu anapozaliwa). Kadhalika, suala hili la ufupi wa maisha, kama litazamwavyo na Jux na Diamond, linajitokeza hata kwa Kezilahabi (1988) katika diwani yake ya *Karibu Ndani* katika shairi la "Waliozaliwa" anapoeleza namna maisha yalivyo mafupi kwa kuyahusianisha na suala la wakati. Mtazamo kama huu pia unadhihirishwa tena na Kezilahabi katika riwaya yake ya *Kichwamaji* (1974). Kezilahabi katika riwaya hii anadhihirisha mtazamo huu kupitia wahusika wake. Katika wimbo huu, licha ya kujidhihirisha kwa mhimili huu, maisha hayasemwi kama ni kifo cha polepole, bali yanatazamwa kuwa ni mafupi. Ufupi huu wa maisha unaozungumziwa, hautofautiani na maisha kutazamwa kama kifo cha polepole ambacho mwanadamu huanza kufa tu pindi anapozaliwa.

Pili, utamaushi unadhihirika katika wimbo uliotafitiwa kwa kuonesha kuwa, licha ya wahusika kukatishwa tamaa na masuala ya mapenzi, suluhu yao siyo kujiua, bali ni kuyafurahia maisha (kujipongeza), kumpenda mama aliyekuzaa na kujipenda mwenyewe. Namna nyingine ya kukabiliana na masuala ya kukatisha tamaa, ikiwamo mapenzi, ni kuelekeza mapenzi kwenye pesa (*kudate* pesa) na kufurahi na marafiki (ma-*home boy*) kwa kuchangamana nao. Nukuu ifuatayo inadhihirisha namna hali ya kukata tamaa inavyojitokeza katika wimbo wa "*Enjoy*":

> Na leo, tena waiteni paparazi
> Warushe kwa mitandao
> **Siyataki mapenzi, nataka jipongeza**
>
> Kama kupenda
> **Bora nimpende mama yangu mmh**
> Kama kupendwa mimi
> **Nitajipenda peke yangu**
>
> **Toka nidate pesa, sasa napendeza**
> **Na tena *naenjoy*, na wanangu mahome boy**
> Ooooh! Akaunti inasoma, na kamwili kananona
> We mwenyewe siunaona?
> Yaani aiii nasema

Wahusika katika wimbo wa "*Enjoy*" wanaonesha suluhu tofauti kabisa katika kukabiliana na mambo yakatishayo tamaa. Suluhu ya namna hii ya kuyafurahia maisha badala ya kujiua kama suluhu ya kuyakatia tamaa maisha inaweza ikaangaziwa katika diwani ya Euphrase Kezilahabi ya *Dhifa* (2008). Katika diwani hii, Kezilahabi anayacheka kabisa maisha. Kukata tamaa ambako ni mojawapo ya mihimili ya udhanaishi kunatokana na kupitia changamoto mbalimbali. Wahusika wa kidhanaishi wanatawaliwa na wazo la kukata tamaa, suala linalosababisha wengi wao kuchukua uamuzi wa kujiua kama suluhu. Mifano ya riwaya ambazo

wahusika wake wanajiua kutokana na kukata tamaa ni Achebe (1958), kupitia riwaya ya *Things Fall Apart* pamoja na Kezilahabi kupitia *Rosa Mistika* (1971) na *Kichwamaji* (1974). Kujiua kama suluhu ya kuyakatia tamaa maisha kunaoneshwa pia na mhusika Cheja katika tamthiliya ya *Hatia* ya Mhando (1972) japo yeye wanajamii wake walimuwahi kabla ya kuchukua uamuzi wa kujiua. Aidha, hali kama hii ya kukata tamaa kwa wahusika wakuu inajidhihirisha katika tamthiliya ya *Pambo* ya Mhando (1975).

Tatu, suala la fujo kama tiba ya utamaushi linadhihirika katika wimbo uliotafitiwa kupitia wahusika kuimba na kucheza kwa furaha. Video ya wimbo huo inaonesha kwamba suala la fujo zisizo na madhara linajitokeza. Wahusika katika wimbo huu wanafurahi kwa kuimba na kucheza huku wakipanda juu ya meza, kucheza kwenye mabwawa ya kuogelea, na kutawanya pesa (tukio la kutawanya pesa katika video ya wimbo huu linaoneshwa na mwanamuziki Diamond Platinumz). Nukuu ifuatayo inadhihirisha namna wahusika wanavyofanya fujo ikiwa ni namna ya kufurahia nafasi waliyo nayo hapa duniani:

> Napenda nikilewa, nipande juu ya meza,
> Minjonjoko natema Kiingereza
> Tupande juu ya meza, tupande juu ya meza
> Tupande juu ya meza, za za za za

Maneno ya nukuu hii yanadhihirisha namna wahusika katika wimbo huu wanavyofurahia kwa kufanya fujo zao kwa njia ya amani kulingana na nafasi waliyo nayo. Wahusika wanapanda juu ya meza. Zaidi, wanaongea lugha ya Kiingereza ili kudhihirisha namna walivyofurahi. Fikra ya nukuu hii kuhusu ‘kuongea Kiingereza’ inasadifu muktadha wa Tanzania, ambapo, mara nyingi, mtu anapolewa huongea maneno ya Kiingereza. Kiitikio

kinadhihirisha namna waimbaji wa wimbo huu wanavyohimiza watu kufurahia maisha (ku*enjoy*) kwa kupoza koo ikiwa na maana ya kupata kinywaji, hususani chenye kilevi. Mhimili (f) wa udhanaishi unaitazama dunia kuwa uwanja wa fujo, ambapo kila mtu amekuja kufanya fujo zake na baadaye atajiondokea na kuwapa nafasi wengine nao waje wafanye fujo zao. Mawazo haya ya kidhanaishi ya kuichukulia dunia kuwa uwanja wa fujo yanajitokeza pia katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) ya Kezilahabi, Mulokozi na Kahigi (1979) katika *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*, Ruhumbika katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo* (1992) na p' Bitek (1972) katika *Song of Lawino* ya p' Bitek (1972). Matendo haya ya fujo huchukuliwa kuwa tiba ya utamaushi kutokana na ukweli kuwa wahusika hufanya hivyo ili kujiepusha na madhara mbalimbali yanayowakuta watu waliotamauka. Kulingana na Fuluge (2022), hali ya kukata tamaa ya maisha huweza kusababisha mtu kupata sonona na hata kujiua.

Nne, utamaushi unadhihirika kupitia kukosekana kwa uaminifu baina ya wapenzi. Katika wimbo wa "*Enjoy*", unaoneshwa uhusiano wa kimapenzi, ambapo mpenzi wa kiume hana furaha kutokana na mpenzi wa kike kutokuwa mwaminifu. Hali hii ya kuyaona mahusiano ya kimapenzi kuwa yamejawa na shubiri haina tofauti na asasi ya ndoa itazamwayo kuwa imegubikwa na huzuni tupu kwani ndoa nayo huhusisha uhusiano wa kimapenzi kati ya mwanamume na mwanamke. Nukuu ifuatayo inadhihirisha namna suala la mapenzi linavyodhihirisha huzuni tupu:

> Nnayemuita huyo *baby*
> Kumbe naye ana *baby*
> Oooh! Unayemwona kipenzi
> Ni mshenzi hakupendi
>
> Ama kweli mtihani
> Mambo mengi duniani
> Na mimi *stress* siwezi
> Ooh! Siwezi

Maneno hayo yanadhihirisha namna mapenzi na ndoa yanavyoonekana kuwa na huzuni tupu. Kulingana na mtazamo wa wadhanaishi, ndoa ni huzuni tupu, na, ikiwa kuna furaha, basi ni kwa kiasi kidogo sana. Shutuma hizo zinazotolewa na msanii Jux katika wimbo huo kuhusiana na mapenzi zinafanana na kile alichokiandika Kezilahabi katika *Kichwamaji* (1974). Kezilahabi (keshatajwa) anatoa mfano wa namna mhusika Kamata alivyopigwa hata kunusurika kifo kisa alikuwa ameoa mwanamke mrembo sana ambaye, watu walipokuwa wanamtongoza, alikuwa akiwakatalia. Wanaume hawa waliona suluhu ya kumpata mke wa Kamata kwa urahisi ni kwa kumuua Kamata ili mke abaki bila mume. Majuto ya Kamata yanadhihirisha namna ndoa ilivyo na huzuni tupu sawa na ambavyo Jux anayashutumu mahusiano ya kimapenzi ambayo yamejaa ulaghai na udanganyifu na kuona suluhu ya mapenzi ya namna hiyo ni kubaki peke yake akifurahia maisha kwa namna nyingine (kwa ku*enjoy*).

Tano, katika wimbo huu, utamaushi unadhihirika kupitia kitendawili cha uhuru wa mwanadamu. Wadhanaishi wanamtazama mwanadamu kama kiumbe asiyekuwa na uhuru. Uhuru wa mwanadamu unatazamwa kuwa una mipaka. Katika wimbo huu wa "*Enjoy*", tunaona wahusika wakiwa na uhuru kupita kiasi tofauti na wahusika wengine wa kazi za kidhanaishi. Haya yanadhihirika katika maneno yafuatayo:

> Napenda nikilewa, nipande juu ya meza
> Minjonjoko natema Kiingereza
> Tupande juu ya meza, tupande juu ya meza
> Tupande juu ya meza, za za za za

Nukuu hii inaonesha kuwa wahusika wana uhuru wa kufanya mambo yao pasipo kizuizi chochote, hali ambayo ni tofauti kabisa na wanavyosawiriwa wahusika wa kidhanaishi. Tukiangalia video ya wimbo huu, tunaona

wahusika wanafurahi na kucheza hata kupanda juu ya meza. Katika kazi zingine za kifasihi za kidhanaishi, wahusika hawana uhuru kama huu. Hali hii inaendana na mawazo ya mhimili wa udhanaishi unaohoji kuhusu dhana ya uhuru binafsi. Je, uhuru wa mtu binafsi upo au haupo? Kwa maana nyingine: je, ni kweli mwanadamu anao uhuru au uhuru wake unadhibitiwa? Pengine, majibu ya maswali haya yanaweza kuwa magumu kulingana na muktadha. Kuna baadhi ya mazingira ambapo uhuru wa mwanadamu kujifanyia mambo yake huweza kudhibitiwa na misingi ya jamii. Katika muktadha mwingine, suala hili huweza kumwonesha mwanadamu kuwa yupo huru kujiamulia kufanya kile anachokitaka. Uhuru huu walio nao wahusika wa "*Enjoy*" haupo kwenye kazi zingine za kisanaa. Kukosekana huko kwa uhuru wa kujiamulia mambo, mathalani, kunajitokeza kwa Rosa katika *Rosa Mistika* (Kezilahabi, 1971) ama Martha katika *Kwenye Ukingo wa Thim* (Hussein, 1997).

**Hitimisho**

Kwa jumla, makala imeonesha namna utamaushi unavyojitokeza katika wimbo wa "*Enjoy*" wa Jux na Diamond. Kuna namna ambavyo utamaushi unaosawiriwa katika wimbo huu unafanana na kutofautiana na maoni ya wadhanaishi wengine. Kwa mfano, wakati wadhanaishi wengine, hususani Kezilahabi, wanaonesha kwamba suluhu ya maisha yaliyokosa maana au suluhu ya kukata tamaa ni kujiua, Jux na Diamond Platinumz wanaamini suluhu ni kuyafurahia maisha. Vilevile, wasanii hawa wanamwona mwanadamu kama kiumbe ambaye yupo huru kujiamulia nini cha kufanya. Hii ni tofauti na wataalamu wengine kama Said na Taib (2019) ambao wanamwona mwanadamu kama kiumbe asiyekuwa na uhuru. Wanamwona mwanadamu kama kiumbe ambaye yupo kifungoni kwani jamii

inayomzunguka na mambo mengine kama mila na desturi yanamtia kifungoni.

Makala inapendekeza kuwa suluhu dhidi ya masuala yakatishayo tamaa haipaswi kuwa kujiua kwani kujiua hakumalizi tatizo husika bali huweza kuibua tatizo jingine. Ni vema kutafuta njia bora ya kukabiliana na masuala yatamaushayo mbali na kujiua. Namna mojawapo ya kukabiliana na masuala ya kukatisha tamaa ni pamoja na kuyafurahia maisha kwa kadri mtu awezavyo au kulingana na nafasi aliyo nayo. Makala inapendekeza pia kuwa, kwa kuwa dunia ni uwanja wa fujo, ni vema fujo azifanyazo mtu ziwe zile za amani. Fujo zinapaswa zisiwaathiri wengine bali, ikiwezekana, ziwe za amani zenye kuwapa manufaa wengine. Uhuru binafsi uzingatie mipaka kwani, kila kitu kinapopitiliza, huweza kuwa na madhara. Kuwapo kwa uhuru wa kujiamulia kuende sambamba na miiko na maadili ya jamii. Kuzingatia mambo haya kutasaidia kuyafanya maisha kuonekana kuwa na maana.

**Marejeleo**

Achebe, C. (1958). *Things Fall Apart*. London: William Heinemann Ltd.

Fuluge, A.N. (2022). Matukio ya Mchakato wa Kujiua katika Riwaya ya *Rosa Mistika*. *Mulika*, Na. 41(2), 145-161.

Hussein, E. (1997). *Kwenye Ukingo wa Thim*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Jux na Diamond Platnumz (2023). *Enjoy*. Dar es Salaam: S2Kizzy.

Kadallah, R.T. (2010). Muziki wa Bongo Fleva na Changamoto za Kimaadili katika Jamii. *Mulika*, 29 & 30, 94-99.

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichwamaji*. Dar es Salaam: East African Publishing House.

Kezilahabi, E. (1975). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Kezilahabi, E. (1988). *Karibu Ndani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (2008). *Dhifa*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Kidashari, F. (2014). *Falsafa ya Udhanaishi katika Hadithi Fupi za Kezilahabi* (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Lupokela A.P. & Msuya M.B. (2010). Dhima ya Bongo Fleva katika Maadili na Malezi kwa Jamii. *Mulika*, 29 & 30, 38-43.

Mahenge, E. (2010). Chimbuko la Muziki wa Hiphop ni Uasi au Sanaa za Maonesho. *Mulika*, 29 & 30, 2-15.

Mhando, P. (1972). *Hatia*. Nairobi: East African Publishing House.

Mhando, P. (1975). *Pambo*. Nairobi: Foudation Books Ltd.

Mulokozi, M.M. & Kahigi, K.K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Omari, S. (2009). *Tanzania Hip Hop Poetry Literature* (Unpublished PhD Thesis). University of Dar es Salaam, Dar es Salaam.

p' Bitek, O. (1972). *Song of Lawino*. Kampala: East African Educational Publishers.

Ruhumbika, G. (1992). *Miradi Bubu ya Wazalendo*. Dar es Salaam: Economic Research Bureau.

Said, Z. na Taib, A.H. (2019). *Fasihi ya Ufungwa: Nadharia na Mikabala ya Uhakiki - Riwaya kama Kifani*. Dar es Salaam: Heko Publishers.

Sakkos, T. (2008). Existentialism and Feminist in Kezilahabi's Novel *Kichwamaji*. *Swahili Forum* 15, 51-61.

Samwel, M. (2012). *Mabadiliko katika Majigambo: Uchunguzi wa Majigambo ya Jadi na ya Bongo Fleva* (Tasinifu ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

TUKI (2010). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K. (1998). Philosophical Labyrinth by Using Two Critical Motifs in Kezilahabi' Prose Works. AAP 55: *Swahili Forum*, V, 79-91.